



# TAARIFA KWA UMMA



## KALENDA YA MATUKIO KWA MWAKA 2023

**Dar es Salaam – Tarehe 23 Januari, 2023**

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) ni Taasisi ya Umma yenye mamlaka ya Kusimamia, Udhhibiti, Utendaji na Ushauri wa kuendeleza na kukuza biashara ya ndani na nje ya nchi ili kuchangia maendeleo ya Taifa.

Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1), (b) (p) cha Sheria Na. 4 ya 2009 kama ilivyorekebisha kwa Sheria Na. 3 ya 2012 kinaipatia TanTrade mamlaka ya kusimamia uratibu wa shughuli za Ukuzaji Biashara ikiwa ni pamoja na Maonesho, Makongamano na Misafara ya Kibiashara.

Kutokana na Wadau kujitokeza kwa wingi katika uandaaji wa Maonesho na Misafara ya Kibiashara nje ya nchi na ili kuleta tija katika shughuli hizi, TanTrade inawaomba Wadau wote nchini wanaojihusisha na uratibu wa shughuli za Ukuzaji Biashara (Trade promotional Events) kama vile Maonesho ya Biashara (Trade Fairs and Exhibitions), Misafara ya Kibiashara (Trade Missions) pamoja na Makongamano ya Kibiashara (Symposiums and Trade Forums) kuwasilisha Kalenda yao ya Matukio yanayotarajiwa kufanyika mwaka 2023 kabla ya 31 Januari, 2023 katika ofisi za TanTrade au kwa barua pepe [info@tantrade.go.tz](mailto:info@tantrade.go.tz)

Kwa maelezo zaidi tafadhali tembelea katika Ofisi zetu zilizopo katika Uwanja wa Maonesho wa Mwl. Nyerere, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam au Jengo la Kilimo V, Barabara ya VETA nyuma ya CBE, Dodoma na Zanzibar, Kijangwani, Jengo la Posta.

Imetolewa na:

David Langa  
Afisa Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma